# KAPSABET HIGH SCHOOL

## SWALI LA LAZIMA

**Ni insha ya kiuamilifu.**

**Sura /mtindo wa tahariri uzingatiwe**

**(1**) Kichwa- Kiandikwe kwa herufi kubwa

**(2)** Jina la gazeti - Msemakweli litumiwe.

**(3**)Tarehe.

**4)**(Jina la mhariri

## Athari za baa la njaa

**(1)** Vifo vya mifugo.

**(2)** Shule kufungwa kutokaba na ukosefu wa chakula.

**(3)** Kuhama kwa jamii kutafuta chakula.

**(4)** Vifo vya binadamu/watu

**(5)** Maradhi mbalimbali kwa mfano utapiamlo.

(**6)** Pato kubwa la kitaifa linatumiwa kushughulikia njaa.

(**7)** Kudumaa kwa maendeleo ya wananchi na taifa.

**(8)** Wanasiasa na mataifa kujinufaisha wakitumia fursa hii.

MWONGOZO 2023

## HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA BAA LA NJAA

**(1)** Wakulima kuhimizwa kupanda mimea inayochukua muda mfupi kukomaa katika sehemu zinazopata mvua chache.

**(2)** Wakulima kupewa mbegu za kupanda bila malipo.

**(3**) Serikali kutangaza baa la njaa kama janga la taifa.

**(4**) Kubuniwa kwa wizara ya mipango maalum inayoshughulikia katizo hili miongoni mwa mengine.

**(5)** Misaada ya chakula kwa wahasiriwa kutoka kwa serikali na wahisani wengine.

**(6)** Serikali kuwahimiza wafugaji kuuza mifugo wao ili kuepuka ukosefu wa nyasi/lishe na maji.

**(7)** Serikali kununua mifugo kutoka kwa wakulima/wafugaji walioathiriwa na baa la njaa.

**(8**) Wakulima kupanda mimea inayoweza kuhimili ukame kama vile mihogo na mtama.

**(9**) Serikali kujenga mabwawa ya maji ili kukusanya maji wakati wa mvua ambapo wakulima wataweza kunyunyizia mimea tao maji wakati wa kiangazi.

**(10)** Serikali kutenga pesa ili kuwezesha shirika la nafaka nchini kununua na kuhifadhi mazao kutoka maeneo yanayojitosheleza kwa mvua.

MWONGOZO 2023

## SWALI LA PILI

## KUUNGA MKONO

(**1**) Shinikizo la rika kuwasukuma vijana kutumia afyuni.

**(2)** Sheria hafifu inayowaruhusu wauzaji na watumizi kuendelea na shughuli zao.

(**3**) kuporomoka kwa maadili ya jamii na kushindwa kwa wazazi kuwathibiti watoto wao kwa kutowapa mawaidha.

**(4)**Ukosefu/ Uchache wa wataalamu wa kutoa nasaha na mwelekeo kwa wanafunzi shuleni.

**(5)** Vyombo vya habari vinachangia pakubwa katika kuwashawishi vinajana kutumia afyuni. Kama vile redio, runinga.

**(6)** Upungufu wa vielelezo/mifano katika jamii.

(**7**) Ufisadi -Wananaowauzia vijana mihadarati hutumia hongo kufanikisha maovu haya.

## KUPINGA.

**(1)** Kutumia sheria kali zitakazowazuia watumiaji na wauzaji wa afyuni kuendeleza shughuli zao.

**(2)** Kuwashauri wazazi kuwa mstari wa mbele kuwazungumzia na kuwashauri watoto wao.

(**3**) Kuthibiti vyombo vya habari katika harakati za kupigana na matumizi ya afyuni.

(**4**) Kuwaajiri na kuongeza wataalamu wa ushauri shuleni na vijijini.

**(5)** Serikali kukabiliana na ufisadi katika vitengo vyote.

**(6)** Kuwashauri wanafunzi kujisimamia kimawazo na kuepuka shinikizo la rika.

**(7)** Vijana kupewa nasaha kuhusu athari za matumizi ya afyuni.

MWONGOZO 2023

**TANBIHI**

**(1**) Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kuunga na moja/zaidi za kupinga.

**(2)** Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kupinga na moja /zaidi za kuunga.

(**3)** Mtahiniwa atoe msimamo wake.

**(4**)Anayekosa kushughulikia pande zote mbili asipitishe alama 10.

**(5)** Mtahiniwa anaweza kutoa hoja sawa pande almuradi atoe msimamo wake.

**(6)** Kadiria hoja zingine za mtahiniwa.

**SWALI LA TATU.**

**1** .Kisa kinafaa kioane na methali

**2.**Mwanafunzi aonyesha sehemu zote mbili za methali.

**3**. Dhana ya mtaka yote ionekane vizuri.

**4.**Dhana ya kukosa yote ijitokeze hata kama ni aya chache au sentensi moja.

**Maana : Anayetaka vitu vingi kwa tamaa hawi na mwisho mzuri.**

**SWALI LA NNE**

**1.** Mtahiniwa aweze kujenga kisa ambacho kinamhusisha yeye mwenyewe kama mhusika mkuu.

**2.** Akimjenga mhusika mkuu mwingine atakuwa anepotoka na hivo basi atuzwe 03/20.

**3.** Mtahiniwa asibadili wakati uliohusika katika swali .Akifanya hivyo atakuwa amepotoka.

MWONGOZO 2023